

02.04.2026

TANGAZO LA ZABUNI YA ULINZI WA MALI ZA UNION MSIMU 2026/2027

Zabuni na: KCU/NC/2026/2027/01

1. Kagera Cooperative Union imetenga fedha kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kimkataba na mtoa huduma ya ulinzi wa mali zake kwa msimu 2026/2027.
2. Kampuni/Shirika mbalimbali la ulinzi linalotambulika linakaribishwa kuleta maombi ya zabuni hii ili kutoa huduma ya ulinzi wa mali pamoja na maghala ya KCU.
3. Kampuni/shirika liambatishe nakala ya usajili wa kampuni
4. Kampuni/shirika liambatishe nakala ya leseni, TIN pamoja na VRN.
5. Kampuni/shirika liambatishe wasifu wake (company profile) ikiwa ni pamoja na kuambatisa nakala ya vyeti vya mafunzo ya ulinzi.
6. Kampuni/shirika liwe na uwezo wa kuwa na walinzi wenye umri usiozidi miaka 50 na wenye uzoefu wa kutumia silaha (**Ambatisha vielelezo**).
7. Mwombaji aambatishe nakala zinaoonesha vielelezo vya kazi alizowahi kufanya.
8. Ombi la zabuni liwe na jina, anwani halisi ya mwombaji na mahali Ofisi ilipo. (Physical address)
9. Maombi yataje gharama zitakazotozwa kwa ajili ya ulinzi bila silaha pamoja na ulinzi kwa kutumia silaha. (**eleza kama ni pamoja na VAT au bila VAT**)
10. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 200,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**
11. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 3-9 vilivyo tajwa hapo juu.
12. Bahasha za maombi zifungwe vizuri kwa lakiri na kuandikwa juu yake:- "**MAOMBI YA ZABUNI YA ULINZI WA MALI ZA UNION MSIMU 2026/2027** kwa anwani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.

13. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.04.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na sherehe ya ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
14. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

MENEJA MKUU
KCU (1990) LTD

